## Neno la Jumatatu, 31. Machi 2014

*Yesu akaomba:*
Sasa roho yangu imefadhaika sana. Niseme nini?
Baba, niokoe na saa hii. Lakini,
ni kwa kusudi hili nimeufikia wakati huu.
*Yohana 12,27*

Mmebarikiwa nata kama
ikiwalazimu kuteseka kwa ajili ya haki.
*1 Petro 3,14*

---

*Jesus prayed:*
Now is my soul troubled. And what shall I say?
“Father, save me from this hour”?
But for this purpose I have come to this hour.
*John 12:27*

Even if you should suffer for righteousness' sake,
you will be blessed.
*1 Peter 3:14 (ESV)*

# Neno Machi 2014
# The Word March 2014

Kiswahili Contemporary Version 2006
English Standard Version

---

Project Bible 2.0 www.bible2.net

## Neno la Jumamosi, 29. Machi 2014

BWANA ni mwema kwa wote,
ana huruma kwa vyote alivyovifanya.
*Zaburi 145,9*

ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni.
Kwa maana Yeye huwaangazia jua lake
watu waovu na watu wema,
naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.
*Mathayo 5,45*

---

The Lord is good to all,
and his mercy is over all that he has made.
*Psalm 145:9 (ESV)*

Your Father makes his sun rise
on the evil and on the good,
and sends rain on the just and on the unjust.
*Matthew 5:45 (ESV)*

## Neno la Jumapili, 2. Machi 2014

Bwana wake akamwambia,
"Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema na mwaminifu!
Umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache,
nitakuweka kuwa msimamizi wa vitu vingi.
Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!"
*Mathayo 25,21*

Basi, watu na watuhesabu sisi kuwa
tu watumishi wa Kristo na mawakili wa siri za Mungu.
Zaidi ya hayo, litakiwalo ni mawakili waonekane kuwa
waaminifu.
*1 Wakorinto 4,1-2*

---

His master said to the servant,
Well done, good and faithful servant.
You have been faithful over a little;
I will set you over much.
Enter into the joy of your master.
*Matthew 25:21 (ESV)*

This is how one should regard us,
as servants of Christ
and stewards of the mysteries of God.
Moreover, it is required of stewards
that they be found trustworthy.
*1 Corinthians 4:1-2 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 27. Machi 2014

Afisa yule alipokuwa bado yuko njiani,
akakutana na watumishi wake wakamwambia kwamba
mwanawe yu mzima.
*Yohana 4,51*

Mwana-Kondoo aliyeko
katikati ya kile kiti cha enzi atakuwa Mchungaji wao,
naye atawaongoza kwenda
kwenye chemchemi za maji yaliyo hai.
Naye Mungu atafuta kila chozi kutoka katika macho yao.
*Ufunuo wa Yohana 7,17*

As the official was going down,
his servants met him
and told him that his son was recovering.
*John 4:51 (ESV)*

The Lamb in the midst of the throne will be their shepherd,
and he will guide them to springs of living water,
and God will wipe away every tear from their eyes.
*Revelation 7:17 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 4. Machi 2014

*Solomoni aomba nyumbani mwa Baba:*
Macho yako na yafumbuke kuelekea hekalu
hili usiku na mchana,
mahali hapa ambapo ulisema,
‘Jina langu litakuwako humo. ’
*1 Wafalme 8,29*

"Mahali hapa nitawapa amani," asema BWANA Mwenye Nguvu.
*Hagai 2,9*

*Solomon prayed in the house of the Lord:*
Your eyes may be open night and day
toward this house, the place of which you have said,
My name shall be there.
*1 Kings 8:29 (ESV)*

In this place I will give peace,
declares the Lord of hosts.
*Haggai 2:9 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 25. Machi 2014

BWANA atakuwa tumaini lako
na kuepusha mguu wako kunaswa katika mtego.
*Mithali 3,26*

Ilipokaribia usiku wa manane,
Paulo na Sila walikuwa wakiomba
na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu,
nao wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.
*Matendo ya Mitume 16,25*

The Lord will be your confidence
and will keep your foot from being caught.
*Proverbs 3:26 (ESV)*

About midnight Paul and Silas were praying
and singing hymns to God,
and the prisoners were listening to them.
*Acts 16:25 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 6. Machi 2014

Mikononi mwako kuna nguvu na uweza kuinua na kuwapa wote nguvu.
*1 Mambo ya Nyakati 29,12*

Watu wote walikuwa wanajitahidi
kumgusa kwa sababu nguvu zilikuwa zikimtoka na kuwaponya wote.
*Luka 6,19*

In your hand are power and might,
and in your hand it is to make great
and to give strength to all.
*1 Chronicles 29:12 (ESV)*

All the crowd sought to touch Jesus,
for power came out from him and healed them all.
*Luke 6:19 (ESV)*

Taken from The Holy Bible, English Standard Version
copyright (c) 2001 by Crossway Bibles,
a division of Good News Publishers.
Used by permission. All rights reserved.

## Neno la Jumapili, 23. Machi 2014

Mungu hutenda mambo makuu kupita ufahamu wetu.
*Ayubu 37,5*

Sasa tunaona taswira kama ya kwenye kioo,
lakini wakati huo tutaona wazi.
Sasa nafahamu kwa sehemu,
wakati huo nitafahamu kikamilifu,
kama vile mimi ninavyofahamika kikamilifu.
*1 Wakorinto 13,12*

---

God does great things that we cannot comprehend.
*Job 37:5 (ESV)*

Now we see in a mirror dimly, but then face to face.
Now I know in part; then I shall know fully,
even as I have been fully known.
*1 Corinthians 13:12 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 8. Machi 2014

Basi ujue kwamba BWANA Mungu wwako ndiye Mungu,
ni Mungu mwaminifu, anayetunza agano la upendo
kwa maelfu ya vizazi vya wale wanaompenda na kuzishika amri zake.
*Kumbukumbu La Torati 7,9*

*Paulo akaandika:*
Kama watenda kazi pamoja na Mungu,
tunawasihi msipokee neema ya Mungu bure bila sababu.
*2 Wakorinto 6,1*

---

Know that the Lord your God is God,
the faithful God who keeps covenant and steadfast love
with those who love him and keep his commandments,
to a thousand generations.
*Deuteronomy 7:9 (ESV)*

*Paul writes:*
Working together with him, then,
we appeal to you not to receive the grace of God in vain.
*2 Corinthians 6:1 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 21. Machi 2014

Ufalme wako ni ufalme wa milele,
mamlaka yako hudumu vizazi vyote.
*Zaburi 145,13*

Ndipo wote waliokuwamo ndani
ya kile chombo wakamwabudu Yesu wakisema,
“Hakika, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.”
*Mathayo 14,33*

---

Your kingdom is an everlasting kingdom,
and your dominion endures throughout all generations.
*Psalm 145:13 (ESV)*

Those in the boat worshiped Jesus, saying,
Truly you are the Son of God.
*Matthew 14:33 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 10. Machi 2014

Kisha BWANA akakifunua kinywa cha punda, akamwambia Balaamu,
“Nimekutendea nini kinachokufanya unipige mara hizi tatu?”
*Hesabu 22,28*

Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa
uchungu kama utungu wa wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa.
*Warumi 8,22*

---

The Lord opened the mouth of the donkey,
and she said to Balaam,
What have I done to you,
that you have struck me these three times?
*Numbers 22:28*

We know that the whole creation has been groaning together
in the pains of childbirth until now.
*Romans 8:22*

## Neno la Jumatano, 19. Machi 2014

Je, maji baridi yatokayo katika
vyanzo vilivyo mbali hukoma kutiririka wakati wowote?
Lakini watu wangu wamenisahau mimi.
*Yeremia 18,14-15*

Laiti ungesikiliza kwa makini maagizo yangu,
amani yako ingekuwa kama mto,
haki yako kama mawimbi ya bahari.
*Isaya 48,18*

---

Do the mountain waters run dry,
the cold flowing streams?
But my people have forgotten me.
*Jeremiah 18:14-15*

Oh that you had paid attention to my commandments!
Then your peace would have been like a river,
and your righteousness like the waves of the sea.
*Isaiah 48:18 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 12. Machi 2014

BWANA ni mwamuzi wetu, BWANA ndiye mtoa sheria wetu,
BWANA ni mfalme wetu, yeye ndiye atakayetuokoa.
*Isaya 33,22*

Vitu vyote vyatoka Kwake, viko Kwake na kwa ajili Yake.
Utukufu ni Wake milele.
*Warumi 11,36*

---

The Lord is our judge; the Lord is our lawgiver;
the Lord is our king; he will save us.
*Isaiah 33:22*

From him and through him and to him are all things.
To him be glory forever.
*Romans 11:36 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 17. Machi 2014

Tazama, amejaa majivuno, anavyovitamani si vya unyofu.
Lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.
*Habakuki 2,4*

Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi.
Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna.
*Wagalatia 6,7*

---

Behold, his soul is puffed up;
it is not upright within him,
but the righteous shall live by his faith.
*Habakkuk 2:4 (ESV)*

Do not be deceived: God is not mocked,
for whatever one sows, that will he also reap.
*Galatians 6:7 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 14. Machi 2014

BWANA akamwambia Abrahamu:
Kwa nini Sara amecheka na kusema,
'Kweli nitazaa mtoto nami sasa ni mzee?'
Je, kuna jambo lo lote gumu lisilowezekana kwa BWANA?
Nitakurudia mwakani majira kama haya,
naye Sara atakuwa na mwana.
*Mwanzo 18,13-14*

Mara Yesu akanyosha mkono Wake na kumshika, akamwambia,
"Wewe mwenye imani haba, kwa nini uliona shaka?"
*Mathayo 14,31*

---

The Lord said to Abraham,
Why did Sarah laugh and say,
"Shall I indeed bear a child, now that I am old?"
Is anything too hard for the Lord?
At the appointed time I will return to you,
about this time next year, and Sarah shall have a son.
*Genesis 18:13-14 (ESV)*

Jesus immediately reached out his hand
and took hold of him, saying to him,
O you of little faith, why did you doubt?
*Matthew 14:31 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 1. Machi 2014

Ee Mungu, kama jina lako lilivyo,
sifa zako zinafika hadi miisho ya dunia.
*Zaburi 48,10*

BWANA ametoa tangazo mpaka miisho ya dunia.
Mwambie Binti Sayuni,"tazama, mwokozi wako anakuja!"
*Isaya 62,11*

---

As your name, O God,
so your praise reaches to the ends of the earth.
*Psalm 48:10 (ESV)*

Behold, the Lord has proclaimed to the end of the earth:
Say to the daughter of Zion,
Behold, your salvation comes.
*Isaiah 62:11 (ESV)*

## Neno la Jumapili, 30. Machi 2014

Ingawa alikuwa Mwana,
alijifunza utii kutokana na mateso aliyoyapata.
*Waebrania 5,8*

Kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili Wake,
ninyi nanyi jivikeni nia iyo hiyo kwa maana mtu aliyekwisha
kuteswa katika mwili ameachana na dhambi.
*1 Petro 4,1*

---

Although Jesus was a son,
he learned obedience through what he suffered.
*Hebrews 5:8 (ESV)*

Since Christ suffered in the flesh,
arm yourselves with the same way of thinking,
for whoever has suffered in the flesh has ceased from sin.
*1 Peter 4:1*

## Neno la Jumatatu, 3. Machi 2014

Msimwache BWANA, bali mtumikieni BWANA kwa moyo
wenu wote.
Msigeukie sanamu zisizofaa. Haziwezi kuwatendea jema,
wala haziwezi kuwaokoa kwa sababu hazina maana.
*1 Samweli 12,20-21*

Namtazama BWANA kwa matumaini,
namngonja Mungu Mwokozi wangu,
Mungu wangu atanisikia mimi.
*Mika 7,7*

---

Do not turn aside from following the Lord,
but serve the Lord with all your heart.
And do not turn aside after empty things
that cannot profit or deliver, for they are empty.
*1 Samuel 12:20-21 (ESV)*

But as for me, I will look to the Lord;
I will wait for the God of my salvation;
my God will hear me.
*Micah 7:7 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 28. Machi 2014

Baada ya siku mbili atatufufua,
katika siku ya tatu atatuinua, ili tuweze kuishi mbele zake.
*Hosea 6,2*

Yesu akawaambia, "Haya ndiyo yaliyoandikwa:
Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu.
Toba na msamaha wa dhambi utatangazwa kupitia Jina
Lake,
kuanzia Yerusalemu."
*Luka 24,46-47*

---

*Hosea called to return to the Lord:*
After two days he will revive us;
on the third day he will raise us up,
that we may live before him.
*Hosea 6:2*

Jesus said to the disciples,
Thus it is written, that the Christ should suffer
and on the third day rise from the dead,
and that repentance and forgiveness of sins
should be proclaimed in his name to all nations,
beginning from Jerusalem.
*Luke 24:46-47 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 5. Machi 2014

Gideoni akauliza, “Ee Bwana wangu, nitawezaje kuwaokoa Israeli?
Ukoo wangu ndio dhaifu kuliko zote katika Manase,
nami ndiye mdogo wa wote katika jamaa yangu.”
*Waamuzi 6,15*

Yeyote amkaribishaye mtoto mdogo kama huyu kwa jina langu,
anikaribisha mimi.
*Mathayo 18,5*

---

*Gideon said to the Lord:*
Please, Lord, how can I save Israel?
Behold, my clan is the weakest in Manasseh,
and I am the least in my father's house.
*Judges 6:15 (ESV)*

Whoever receives one such child in my name receives me.
*Matthew 18:5 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 7. Machi 2014

Neno langu halitanirudia tupu,
bali litatimiliza lile nililokusudia
na litafanikiwa katika kusudi lile nililolituma.
*Isaya 55,11*

*Yesu aambia Umati kuhusu Mfano wa Mpanzi*
Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri
ambapo zilitoa mazao, nyingine mara mia moja,
nyingine mara sitini na nyingine mara thelathini.
*Mathayo 13,8*

---

My word shall not return to me empty,
but it shall accomplish that which I purpose,
and shall succeed in the thing for which I sent it.
*Isaiah 55:11 (ESV)*

*Jesus said in the parable of the sower:*
Other seeds fell on good soil and produced grain,
some a hundredfold, some sixty, some thirty.
*Matthew 13:8 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 26. Machi 2014

Mungu si mtu
Je, anasema, kisha asitende? Je, anaahidi, asitimize?
*Hesabu 23,19*

*Kristo akasema:*
Mimi ndimi njia na kweli na uzima.
Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu.
*Yohana 14,6*

---

Has God said, and will he not do it?
Or has he spoken, and will he not fulfill it?
*Numbers 23:19 (ESV)*

*Christ says:*
I am the way, and the truth, and the life.
No one comes to the Father except through me.
*John 14:6 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 24. Machi 2014

Daudi akajitia nguvu katika BWANA, Mungu wake.
*1 Samweli 30,6*

Wanafunzi Wake wakamwambia Bwana, “Tuongezee imani.”
*Luka 17,5*

---

David strengthened himself in the Lord his God.
*1 Samuel 30:6 (ESV)*

The apostles said to the Lord,
Increase our faith!
*Luke 17:5 (ESV)*

---

Scriptures taken from Kiswahili Contemporary Version
Copyright (c) 1984, 1989, 2006 by International Bible Society(R)
Used by permission.  All rights reserved worldwide.

## Neno la Jumapili, 9. Machi 2014

Umenitenga na rafiki zangu na kunifanya wanisukumie mbali.
Nimezuiliwa wala siwezi kutoroka.
*Zaburi 88,8*

*Mungu asema:*
Ataniita, nami nitamjibu,
nitakuwa pamoja naye katika taabu,
nitamwokoa na kumheshimu.
*Zaburi 91,15*

---

You have caused my companions to shun me;
you have made me a horror to them.
I am shut in so that I cannot escape.
*Psalm 88:8 (ESV)*

*The Lord says:*
When he calls to me, I will answer him;
I will be with him in trouble;
I will rescue him and honor him.
*Psalm 91:15 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 22. Machi 2014

Wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri,
hulisikia lile neno, wakalipokea na kutoa mazao:
Wengine thelathini, wengine sitini na wengine
mara mia moja ya ile iliyopandwa.
*Marko 4,20*

*Kristo akasema:*
Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi.
Akaaye ndani Yangu,
nami ndani yake,
huyo huzaa sana,
maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya jambo lo lote.
*Yohana 15,5*

---

Those that were sown on the good soil
are the ones who hear the word
and accept it and bear fruit,
thirtyfold and sixtyfold and a hundredfold.
*Mark 4:20 (ESV)*

*Jesus said:*
I am the vine; you are the branches.
Whoever abides in me and I in him,
he it is that bears much fruit,
for apart from me you can do nothing.
*John 15:5 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 11. Machi 2014

Nitatia Roho yangu ndani yenu nanyi mtaishi,
nami nitawakalisha katika nchi yenu wenyewe.
Ndipo mtakapojua kwamba mimi BWANA.
*Ezekieli 37,14*

Basi hatukupokea roho ya dunia bali Roho yule atokaye kwa Mungu,
ili tuweze kuelewa kile kipawa ambacho Mungu ametupatia bure.
*1 Wakorinto 2,12*

---

I will put my Spirit within you,
and you shall live,
and I will place you in your own land.
Then you shall know that I am the Lord.
*Ezekiel 37:14 (ESV)*

We have received not the spirit of the world,
but the Spirit who is from God,
that we might understand
the things freely given us by God.
*1 Corinthians 2:12 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 20. Machi 2014

Nimeyasikia maombi yako na kuona machozi yako.
*2 Wafalme 20,5*

Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao.
Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio,
wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza
yamekwisha kupita.
*Ufunuo wa Yohana 21,4*

---

I have heard your prayer;
I have seen your tears.
*2 Kings 20:5 (ESV)*

God will wipe away every tear from their eyes,
and death shall be no more,
neither shall there be mourning,
nor crying, nor pain anymore,
for the former things have passed away.
*Revelation 21:4 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 13. Machi 2014

Afadhali kuwa na kidogo pamoja na kumcha BWANA,
kuliko mali nyingi pamoja na ghasia.
*Mithali 15,16*

Yesu alipoinua macho yake, aliwaona matajiri wakiweka
sadaka zao kwenye sanduku la hazina ya hekalu.
Akamwona pia mwanamke mmoja mjane maskini,
akiweka humo sarafu mbili za shaba.
Yesu akasema, "Amin, amin nawaambia, huyu mjane maskini ameweka
humo sadaka kubwa zaidi kuliko wengine wote."
*Luka 21,1-3*

---

Better is a little with the fear of the Lord
than great treasure and trouble with it.
*Proverbs 15:16 (ESV)*

Jesus looked up and saw the rich
putting their gifts into the offering box,
and he saw a poor widow put in two small copper coins.
And he said, “Truly, I tell you,
this poor widow has put in more than all of them.”
*Luke 21:1-3 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 15. Machi 2014

Jihadharini, la sivyo mtashawishika kugeuka
na kuabudu miungu mingine na kuisujudia.
*Kumbukumbu La Torati 11,16*

Kwa sababu mahali akiba yako ilipo,
hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa.
*Mathayo 6,21*

---

Take care lest your heart be deceived,
and you turn aside and serve other gods and worship them.
*Deuteronomy 11:16 (ESV)*

Where your treasure is,
there your heart will be also.
*Matthew 6:21 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 18. Machi 2014

Mungu ameona taabu yangu na kazi ngumu ya mikono yangu.
*Mwanzo 31,42*

Simameni imara, msitikisike,
mzidi sana katika kuitenda kazi ya Bwana,
kwa maana mnajua ya kuwa, juhudi yenu si bure katika Bwana.
*1 Wakorinto 15,58*

---

God saw my affliction
and the labor of my hands.
*Genesis 31:42 (ESV)*

Be steadfast, immovable,
always abounding in the work of the Lord,
knowing that in the Lord your labor is not in vain.
*1 Corinthians 15:58 (ESV)*

## Neno la Jumapili, 16. Machi 2014

Simoni Petro akamjibu, “Bwana, tuondoke twende kwa nani?
Wewe unayo maneno ya uzima wa milele.
Tunaamini na kujua kuwa Wewe
ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai.”
*Yohana 6,68-69*

Kwa hiyo, vifungeni viuno vya nia zenu,
mwe na kiasi,
mkitumainia kikamilifu ile neema mtakayopewa,
Yesu Kristo atakapodhihirishwa.
*1 Petro 1,13*

---

Simon Peter answered Jesus,
Lord, to whom shall we go?
You have the words of eternal life,
and we have believed, and have come to know,
that you are the Holy One of God.
*John 6:68-69 (ESV)*

Set your hope fully on the grace
that will be brought to you
at the revelation of Jesus Christ.
*1 Peter 1:13 (ESV)*